*Mulika, Na. 43 (1), 175-195*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Uchambuzi wa Mitindo ya Kiepisto katika Riwaya za Kiswahili: Aina na Matumizi ya Lugha

*Yusta Violet Mganga*[1]
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
na
*Leonard Flavian Ilomo*[2]
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na43t1.10

**Ikisiri**

Fasihi inapitia mabadiliko na kupata maendeleo katika matumizi ya mitindo ya uandishi wa kazi za fasihi. Baadhi ya mitindo hii inajulikana kama mitindo ya kiepisto. Vinogradu na Skuortson (2014) wameeleza kuwa miongoni mwa mitindo ya kiepisto inayotokana na mawasiliano ya kielektroniki ni kama arafa, baruapepe, blogu, wakati mawasiliano kila siku ndani ya jamii ni kama vile barua na shajara. Mitindo hii imezoeleka kukidhi mawasiliano katika miktadha mbalimbali (Vinogradu na Skuortson, 2014). Kumekuwa na matumizi ya mitindo ya kiepisto katika kazi za fasihi. Mmojawapo wa wataalamu waliojadili mitindo ya kiepisto katika fasihi ni Mutembei (2016) aliyechunguza dhima ya mitindo ya kiepisto katika fasihi ya Kiingereza na Kiswahili, na kubaini matumizi ya mtindo wa kiepisto wa barua ingawa mitindo ya kiepisto ni mingi. Kutokana kutokuwa na maelezo ya kutosha ya kiutafiti kuhusu aina za mitindo ya kiepisto, makala haya yamechunguza mitindo ya kiepisto katika fasihi ya Kiswahili ili kubaini aina zake, na vipengele vya matumizi ya lugha katika mitindo hiyo. Data za mjadala huu zilipatikana maktabani kupitia usomaji makini. Nadharia ya Usemezano ya Bahktin (1980) na Nadharia ya Mtindo ya Leech (1969) zimetumika. Makala haya yalibaini mitindo ya kiepisto iliyotokana na mawasiliano ya kielektroniki kama: arafa, na baruapepe. Vilevile, mawasiliano yaliyotokana na nyaraka za mawasiliano ya kawaida kama: barua na shajara. Pia, makala haya yalibaini vipengele mbalimbali vya matumizi ya lugha vilijitokeza kama tashibiha, tasfida, majazi, taashira, methali, misemo na nahau kudhihirisha sanaa iliyomo katika mitindo ya kiepisto.

## 1.0 Utangulizi

Neno ‘episto’ limetokana na neno “*epistle*” katika lugha ya Kigiriki linalomaanisha “barua” na linatokana na kitenzi “*epistellein*” chenye maana ya ‘kutuma kwa au kwenda kwa’ (Aşci, 2020). Mitindo ya kiepisto ilianza na uchopekwaji wa nyaraka za mawasiliano ya kawaida ndani ya jamii kama barua na shajara katika karne ya 16 na 17. Ilipofikia karne ya 19, mitindo ya kiepisto ilipiga hatua ya maendeleo na

[1] **Baruapepe:** mgangay15@gmail.com
[2] **Baruapepe:** ilomo.leonard@udsm.ac.tz

kuhusisha mawasiliano ya kielektroniki kama arafa, baruapepe, blogi katika kazi za fasihi (Couldry na Mc Carthy, 2004). Katika fasihi ya Kiswahili mitindo mbalimbali hutumika, miongoni mwa mitindo hiyo ni matumizi ya mawasiliano ya kielektroniki kama arafa, baruapepe na blogu. Pia, nyaraka nyingine za mawasiliano ya kila siku ndani ya jamii kama shajara na baruapepe. Mitindo hii hujulikana kama mitindo ya kiepisto (Mutembei, 2016).

Dhana ya mtindo imejadiliwa na wataalamu mbalimbali. Miongoni mwao ni Mwansoko (1991), Senkoro (2011), Jilala (2016) na Mulokozi (2017). Wataalamu hao wamefasili na kufafanua dhana ya mtindo kwa mitazamo tofauti. Mwansoko (1991) anauelezea mtindo kuwa ni mfumo wa zana za kilugha unaotokana na maendeleo ya kukua kwa lugha ambao hutofautiana kufuatana na kutumiwa kwake katika mawasiliano yanayohusu nyanja mbalimbali za kazi na shughuli za jamii. Hii ina maana kwamba mtindo ni zana inayotokana na maendeleo ya lugha na hutumika katika mawasiliano mbalimbali katika jamii. Mtazamo huu umejikita zaidi katika isimujamii. Senkoro (2011) akinukuliwa na Madumulla (2022: 148) anaeleza: "mtindo ni matumizi ya lugha ya aina aina. Humu tunagundua tamathali za usemi, misemo, nahau, methali, uchaguzi wa msamiati, miundo ya sentensi, ufundi wa kuwachora au kuwaeleza wahusika, mandhari na matukio, na hata utamu wa lugha. Pia, kuna masuala ya vipeo, pamoja na ucheshi, matumizi ya komedia na utanzu ndani ya utanzu. Yote yanapaswa kuchunguzwa namna yalivyotumika kuchangia katika kukamilisha kazi ya fasihi". Mawazo haya hayatofautiani sana na mawazo ya Mwansoko (1991) kuwa mtindo ni matumizi ya lugha, lakini Senkoro (2011) ameuelezea mtindo zaidi kwa kubainisha vipengele vya matumizi ya lugha ambavyo hudhihirisha mtindo.

Naye Jilala (2016) anaeleza kuwa mtindo hujibainisha katika vipengele anuwai kama mpangilio wa sentensi, matumizi ya tamathali, usawiri wa wahusika, motifu, dhamira na mbinu za usimulizi. Jilala (2016) ana mawazo yanayofanana na ya Senkoro (2011) ingawa yeye ameongeza kipengele cha motifu na dhamira. Vilevile, Mulokozi (2017) amefafanua dhana ya mtindo kwa mtazamo tofauti na watalaamu waliokwishatajwa hapo juu. Yeye anaeleza kuwa mwandishi wa kazi ya fasihi huamua asimulie kisa chake kwa mtindo fulani, wa moja kwa moja, wa urejelezi, wa udokezi, wa mafumbo, wa kiistiara au wa barua. Mtaalamu huyu, ameelezea mtindo kwa mtazamo wa matumizi ya mbinu za usimulizi. Kwa kuzingatia mawazo ya Mwansoko (1991) ya kuwa mtindo huweza kuwa tofauti kutegemea kipindi, wakati, na miongo, pamoja na mawazo ya Mulokozi (2017) kuwa mwandishi wa kazi ya fasihi huamua asimulie kisa chake kwa mtindo fulani, hivi sasa tunashuhudia mitindo iliyoibuka kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Mitindo hii inatokana na mawasiliano ya kiektroniki kama arafa, baruapepe na blogi na hupachikwa katika kazi za fasihi. Baada ya kuangalia dhana ya mtindo kutoka kwa wataalamu mbalimbali, katika utafiti huu tulitumia mtazamo wa Senkoro

(2011) ambao ulijikita katika kuchunguza vipengele vya matumizi ya lugha ili kubaini sanaa iliyomo katika kazi ya fasihi.

Aidha, tumeshuhudia mitindo inayoendana na mabadiliko kwenye jamii katika uandishi wa kazi za fasihi. Walibora (2010) anaeleza kwamba riwaya za Kiswahili zimepiga hatua katika mitindo kiasi cha kuendana na mabadiliko yanayotokea katika jamii. Mutembei (2016) amehakiki mitindo ya kiepisto katika fasihi ya Kiingereza na Kiswahili kuchunguza nguvu ya mawasiliano dhidi ya ukimya. Mutembei anaeleza kuwa mitindo ya kiepisto ilianza na barua pamoja na shajara zilizochopekwa katika riwaya mwaka 1485 na kushamiri katika karne ya 18. Hata hivyo, kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, ilipofika karne ya 19, mitindo hiyo ilihusisha mawasiliano ya kielektroniki kama arafa, baruapepe na blogu. Mutembei anashauri kuwa ingawa mitindo hii imeonesha kushamiri katika vipindi tofauti, bado tafiti zaidi zinahitajika ili kubaini ujitokezaji wake kwenye tanzu za fasihi.

Tafiti zimefanywa kuhusu mitindo ya kiepisto katika fasihi kwa ujumla. Tafiti hizi zimejikita kuchunguza mtindo wa kiepisto wa barua na dhima yake katika jamii (taz. Dagel, 2012; Ondus, 2014 na Mutembei, 2016). Zaidi ya tafiti hizo, kwa uelewa wa wetu, bado hakuna maelezo ya kina ya kiutafiti katika fasihi ya Kiswahili kuhusu aina za mitindo ya kiepisto. Hali hii imezua maswali iwapo kila mawasiliano ndani ya jamii, na kila mawasiliano ya kiektroniki huweza kutumika kama mtindo wa kiepisto. Kukosekana kwa maelezo ya kiutafiti kuhusu mitindo ya kiepisto kumechangia kukosekana kwa tafiti za kutosha kuhusu mitindo ya kiepisto katika fasihi ya Kiswahili. Kwa kuzingatia hilo, tafiti zilizofanywa kuhusu mitindo ya kiepisto hazijaweza kutoa ithibati toshelevu kuhusu aina ya mitindo ya kiepisto. Kwa mantiki hiyo, makala haya yanabainisha aina za mitindo ya kiepisto katika fasihi ya Kiswahili na kuelezea jinsi lugha ilivyotumika katika mitindo hiyo.

## 2.0 Mbinu za Ukusanyaji Data

Data zilizotumika katika makala haya zilipatikana kutoka katika utafiti uliofanyika maktabani. Katika kufanikisha mchakato wa ukusanyaji data, mtafiti alitumia mbinu ya usampulishaji nasibu ambayo ilimuwezesha kupata riwaya zifuatazo: *Dunia Uwanja wa Fujo* ya Euphrase Kezilahabi (1975 [2007])[3]; *Mikidadi wa Mafia, Maisha ya Mwanaharakati na Familia yake Nchini Tanzania* ya Pat Caplan (2014) iliyotafsiriwa kwa Kiswahili na Ahmad Kipacha (2014); *Kolonia Santita* ya Enock Maregesi (2017), na *Maji Hayafuati Mkondo* ya Felistas Mahonge (2018).

Data za msingi zilikusanywa kwa mbinu ya kusoma kwa kina riwaya teule na kudurusu machapisho yaliyohusu mitindo ya uandishi wa kazi za fasihi. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Usemezano, data zilizohusu lengo la kwanza ambalo ni

[3] Utafiti huu umetumia toleo la mwaka 2007.

kubainisha aina za episto zilipangwa katika makundi mawili. Kundi la kwanza lilihusu aina za mitindo inayotokana na mawasiliano ya kila siku katika jamii, na kundi la pili lilihusu aina za episto zinazotokana na mawasiliano ya kielektroniki. Baada ya hapo, kwa kuongozwa na Nadharia ya Mtindo, data zilizohusu lengo la pili ambalo ni kuelezea vipengele vya matumizi ya lugha katika mitindo ya kiepisto lilishughulikiwa katika makundi yote. Kupitia hatua hizo tulifanikiwa kufikia malengo ya utafiti.

**3.0 Mwega wa Kinadharia**

Utafiti uliongozwa na nadharia mbili, Nadharia ya Usemezano na Nadharia ya Mtindo, kwa sababu zina mwelekeo wa kuchunguza mtindo wa kilichoandikwa na jinsi kilivyoandikwa. Kwa hiyo, nadharia hizi mbili zimefaa utafiti huu uliolenga kuchunguza mitindo ya kiepisto katika fasihi ya Kiswahili.

Nadharia ya Usemezano iliasisiwa na Mikhaila Mikhailovik Bakhtin (1981) ambaye alikuwa na wafuasi wengi kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007). Miongoni mwao ni Gary Marson (1986), Michael Holquist (1990) na Kimani Njogu (2004). Wamitila (2008) anaeleza kuwa mawazo ya Bakhtin yalikua, kuenea na hatimaye kumfanya ajulikane kama mhakiki mwishoni mwa karne ya ishirini. Bakhtin (1981) amejikita katika kuangalia urejelewaji wa mawazo ndani ya matini ya kifasihi au nje ya matini. Bakhtin (1981) anaamini kuwa asili ya mazungumzo katika lugha imetoa fursa za kutumia sauti za pande nyingi katika aina nyingi za uandishi. Bakhtin ameeleza kuwa mwandishi Fyodor Dostoevsky ndiye mwasisi wa riwaya ya kipolifoni (*polyphony*). Riwaya za kipolifoni hudhihirisha uwepo wa sauti nyingi tofauti zilizo huru ambazo huruhusu maana nyingi. Bakhtin (1981) anaamini kuwa hakuna matini inayoweza kujitegemea peke yake bila kuhusisha matini nyingine. Katika *Dialogic Imagination*, Bakhtin (1981) anaeleza kuwa riwaya ina sifa tano muhimu ambazo hudhihirisha usemezano. Sifa hizo ni: mosi, kuwa na masimulizi tofauti ya kifasihi ya moja kwa moja kutoka kwa mwandishi; pili, kuwa na mitindo ya njia mbalimbali za masimulizi ya kila siku yaliyosemwa au yaliyoandikwa kama barua na shajara; tatu, kuwa na mitindo ya njia mbalimbali za masimulizi ya kila siku ya kiusemezano; nne, kuwa na mitindo ya njia mbalimbali za mawasiliano zilizo na sanaa ya kiwango cha juu kutoka kwa mwandishi na uzungumzi nafsia wa wahusika; na tano, sifa zote hizi huingiliana na kuhusiana katika riwaya ili kuunda riwaya nzima kwa kuingiliana na lugha yake na zinapatikana kwa kiwango kikubwa katika riwaya, hazipatikani katika tamthilia na ushairi.

Katika kuchunguza aina za episto zilizojitokeza katika riwaya teule, tuliongozwa na mihimili mitatu. Kwanza, ni kuwapo kwa masimulizi tofauti ya kifasihi ya moja kwa moja kutoka kwa mwandishi na kuwa na mitindo ya njia mbalimbali za masimulizi ya kila siku ambayo yameandikwa kama vile barua na shajara. Pili, ni kuwapo kwa mitindo ya njia mbalimbali za mawasiliano zilizo na sanaa ya kiwango cha juu kutoka kwa mwandishi na uzungumzi nafsia wa wahusika katika kubaini

mitindo ya arafa, baruapepe na blogu. Tatu, sifa zote zinaingiliana na kuhusiana katika kuunda riwaya nzima katika kujumuisha matumizi ya mitindo mbalimbali katika riwaya teule. Katika utafiti huu, riwaya teule zimedhihirisha kuingiliana na kutegemeana kwa matini mbalimbali na kuunda riwaya nzima.

Kwa upande wa Nadharia ya Mtindo, Marumba (2013) anaeleza kuwa nadharia hii iliasisiwa na Leech (1969), na hutumika katika uhakiki wa fasiri ya matini kwa mtazamo wa kiisimu na kitaaluma unaofungamana na uhakiki wa kifasihi na kiisimu. Anaendelea kueleza kuwa mtindo hubainisha kanuni za kueleza uteuzi mahususi unaofanywa na mwandishi katika matumizi ya lugha kuhusu utoaji na upokeaji wa maana, uhakiki wa kidiskosi, uhakiki wa kilongo na wa kifasihi. Aidha, athari ya matini yoyote hutokana na mtindo ambao huonesha jinsi lugha inavyotumiwa, na mwandishi huchagua namna ya kuwasilisha mawazo yake. Aidha, wataalamu mbalimbali wamechangia mawazo kuboresha nadharia hii, miongoni mwao ni Cystal na Davy (1981), Wamitila (2008), Leech na Short (2007) na Simpson (2004) kwa kuwataja wachache. Cystal na Davy (1981) wameongezea upande wa sifa za lugha na kuziweka katika kategoria kulingana na sifa hizo kimuktadha. Pia, Wamitila (2008) anaunga mkono mawazo ya Leech (1969) na kuongezea kuwa nadharia hii huweza kuhakiki vipengele vya fani na maudhui katika kazi za fasihi.

Vilevile, Leech na Short (2007) wameboresha nadharia hii kwa kubainisha viwango vya aina za ukiushi wa kaida za matumizi ya lugha ambavyo hutumika katika uhakiki wa mitindo ya kazi za fasihi. Naye Simpson (2004) anaunga mkono mawazo ya Leech (1969) kuhusu viwango vya ukiushi na kuorodhesha vipengele vya msingi ambavyo vinafaa kufuatwa wakati wa uhakiki. Kulingana na mawazo ya wataalamu hawa, misingi inayofaa kuhakiki mtindo ni: msingi wa maandishi, wa umbo, wa kisarufi, wa kisemantiki, wa uwasilishaji wa mawazo, wa masimulizi, na mwisho ni msingi wa kiitikadi na mtindo. Katika kutathmini matumizi ya lugha katika mitindo ya kiepisto, utafiti huu ulitumia msingi wa kisemantiki unaohusu lugha ya kitamathali na miundo ya lugha. Msingi huu hujikita kuchunguza jinsi matumizi ya maneno ya lugha yanavyoathiri maana. Ukiushi wa aina hii unahusu matumizi ya maneno kwa njia ambazo si za kawaida kimaana kama inavyofasiriwa katika hali ya kawaida.

## 4.0 Muhtasari wa Riwaya Teule

*Dunia Uwanja wa Fujo* (2007) ni riwaya iliyoandikwa na Euphrase Kezilahabi. Ilichapishwa kwa mara ya kwanza mnamo mwaka 1975. Riwaya hii inazungumzia kisa cha Tumaini, kijana anayekulia katika mazingira ya utajiri katika kijiji kilichotamalaki umaskini, ushirikina na vituko kabla ya kuhamia mjini na kukumbana na ulimwengu tofauti na aliouzoea. Riwaya hii inaonesha jinsi maisha ya Tumaini yanavyoingiliana na wahusika wengine katika jamii yake inayokumbwa na mabadiliko ya kijamii na kisiasa. Aidha, riwaya hii imeonesha msako wa furaha

maishani unavyoweza kukumbwa na kila aina ya vikwazo na suala la malezi lilivyo changamoto miongoni mwa jamii ya leo.

*Mikidadi wa Mafia, Maisha ya Mwanaharakati na Familia yake Nchini Tanzania* ya Pat Caplan (2014), iliyotafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Ahmad Kipacha (2014), ni riwaya inayozungumzia maisha ya Mikidadi tangu alipokuwa kijana hadi kifo chake. Riwaya hii inahusu harakati za mhusika mkuu, Mikidadi, za kutafuta elimu, maisha yake ya ndoa na familia, harakati za kimaisha na ushiriki wake katika siasa, maendeleo ya kisiwa cha Mafia katika milenia mpya, kifo cha Mikidadi, na mustakabali wake. Mwisho, riwaya hii inazungumzia mabadiliko katika kisiwa cha Mafia tangu mwaka 1965 hadi mwaka 2010.

Riwaya nyingine ni *Kolonia Santita* (2017) iliyoandikwa na Enock Maregesi. Riwaya hii ina hadithi ya kusisimua ya kijasusi inayohusu muhtasari wa mauaji ya kinyama yaliyotokea nchini Meksiko. Mauaji hayo yalikuwa baina ya Tume ya Dunia ya Umoja wa Mataifa ya kudhibiti dawa za kulevya na ugaidi wa kimataifa; na shirika kubwa la dawa za kulevya la Kolonia Santita la Kolumbia na Meksiko. Mauaji hayo yamechochea hofu na mtafaruku mkubwa katika jamii na vyombo vya habari na ujasusi duniani, na kusababisha shinikizo kubwa kwa viongozi wa dini na serikali pamoja na wananchi kwa ujumla. Kutokana na mauaji hayo, viongozi na wananchi wanaonekana wamepoteza imani na Tume ya Dunia ya Umoja wa Mataifa. Aidha, tatizo halikuwa dawa za kulevya pekee; jambo la hatari na baya zaidi kwa amani ya dunia ni Kolonia Santita kuwa na malighafi ya nyuklia, *Plutonium* - 239, katika msitu wa *Amazon* nchini Kolumbia, iliyoibiwa na mwanafizikia wa Kolonia Santita katika jiji la *New Mexico*, nchini Marekani. Kiongozi wa Tume ya Dunia hajui ataeleza nini kwa Umoja wa Mataifa. Hajui atasema nini kwa wahisani wa Tume kuhusiana na ufisadi wa Kolonia Santita.

Aidha, *Maji Hayafuati Mkondo* (2018) ni riwaya iliyoandikwa na Felista Mahonge ambayo inazungumzia changamoto zinazowapata wanawake katika kufikia ndoto za maisha yao. Katika riwaya hii tunawaona wahusika Mama Sita na Mercy wakiwa wanawake wenye utashi mkubwa wa kupambanua mambo kwa ujasiri mkubwa katika changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo wanawake mpaka kufikia ndoto zao maishani. Pia, wahusika hawa wamechorwa kuonesha mchango wa wanawake katika kuijenga familia kimaadili na kiuchumi. Kupitia wahusika hawa, mwandishi anasisitiza umuhimu wa wazazi kushiriki pamoja katika malezi ya watoto na kuijenga familia kwani ndiyo mhimili wa taifa la kesho. Mwandishi anapiga vita wazazi na walezi ambao wanashiriki kwa makusudi katika kuangamiza kizazi kipya. Anakemea suala la matumizi ya dawa za kulevya, biashara ya binadamu pamoja na rushwa. Pia, mwandishi katika riwaya hii, anaonesha umuhimu wa vyombo vya dola katika kusimamia haki za wanaodhulumiwa katika jamii.

## 5.0 Aina za Mitindo ya Kiepisto

Mitindo ya kiepisto iliyojitokeza katika riwaya teule imetokana na mawasiliano ya kila siku ndani ya jamii, mtindo wa barua na shajara. Barua zimejitokeza katika riwaya teule tatu kati ya nne zilizoteuliwa. Shajara zimejitokeza katika riwaya teule mbili kati ya nne zilizoteuliwa. Vilevile, mtindo uliotokana na mawasiliano ya kielektroniki wa baruapepe umejitokeza katika riwaya teule moja kati ya nne zilizoteuliwa. Barua zimedhihirika katika riwaya zifuatazo: *Dunia Uwanja wa Fujo* (2007), *Mikidadi wa Mafia: Maisha ya Mwanaharakati na Familia yake Nchini Tanzania* (2014) na *Maji Hayafuati Mkondo* (2018) kama jedwali hapo chini linavyoonesha;

**Jedwali Na. 1: Data kuhusu Ujitokezaji wa Barua za Kawaida**

| Riwaya Teule | Idadi ya Barua | Kategoria | Aina za Barua |
|---|---|---|---|
| *Dunia Uwanja wa Fujo* (2007) | 7 | Barua za kubuni | Barua za kirafiki |
| *Mikidadi wa Mafia: Maisha ya Mwanaharakati na Familia yake Nchini Tanzania* (2014) | 59 | Barua halisi | Barua za kirafiki na kikazi |
| *Maji Hayafuati Mkondo* (2018) | 3 | Barua za kubuni | Barua za kirafiki |

**Chanzo:** *Dunia Uwanja wa Fujo* (2007), *Mikidadi wa Mafia: Maisha ya Mwanaharakati na Familia yake Nchini Tanzania* (2014) na *Maji Hayafuati Mkondo* (2018)

Data za utafiti kutoka katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (2007) zimedhihirisha matumizi ya barua kati ya Dennis na Vera ambao walikuwa wakisoma darasa moja hadi walipofika darasa la kumi na mbili. Baada ya kuhitimu darasa la kumi na mbili, Dennis alikwenda Kivukoni na Vera alikwenda kozi ya ukarani na kuanza kazi mapema kabla ya Dennis. Vera alikuwa msichana mwenye sifa ya utukutu tangu alipokuwa shuleni. Alipofikisha miezi saba kazini, alipata ujauzito kama barua ifuatayo inavyoeleza:

> "Dennis kuna wanafunzi wawili wa Chuo Kikuu ambao wamekwishanisumbua. Wanataka uchumba na mimi. Mimi nimewakataa wote kwa ajili yako, ninakungoja wewe. Ufahamu Dennis tangu zamani nilijizuia kufanya lolote pamoja na wewe kwa kuwa nilifahamu kwamba wewe ndiye uliyekuwa mchumba wangu wa pekee… Siku niliyokuona huko mjini Dar es Salaam ulikuwa umekwishabadilika. Ulikuwa mzuri sana machoni mwangu. Moyo wangu ulikuwa na njaa yako vile

> kwamba sikuweza kuvumilia. Nilitoa chochote nilichokuwanacho. Labda maji ya bahari ndiyo yamekufanya uwe mweupe vile! Dennis mambo yalitendeka Rex Hotel. Wakati ninapoandika barua hii nimechukua mali yako tumboni mwangu. Ukinitupa sasa, basi, maisha yangu yameharibika.
> Sina mengi, pokea picha yangu V" (Kezilahabi, 2007: 68).

Dondoo hilo la barua linadhihirisha matumizi ya barua ya kubuni, barua ya kirafiki. Barua hii haina anwani ya mwandikaji, haina tarehe, imeanza na jina la mwandikiwa Dennis, na kufuatiwa moja kwa moja na kiini cha barua yenyewe. Mwishoni haina jina bali imehitimishwa na sentensi ifuatayo: "Sina mengi, pokea picha yangu" (Kezilahabi, 2007: 68). Barua hii inampasha habari Dennis kuhusu hali ya Vera tangu aondoke Dar es Salaam. Barua za kirafiki huwa hazina kichwa cha habari, mwanzo wake hauhitaji wadhifa wa mwandikiwa. Barua za kirafiki zina uhuru wa kutumia lugha yoyote, kama vile maneno ya mitaani au mzaha kutegemeana na maudhui yake, uhusiano baina ya mwandishi na mwandikiwa. Ujitokezaji wa barua hii katika hadithi kuu, unadhihirisha kuwapo kwa sauti nyingi zilizo huru. Aidha riwaya hii, imehusisha uchopekwaji wa barua 7 katika hadithi kuu. Hivyo, riwaya hii imedhihirisha matumizi ya mawasiliano ya kawaida ya kila siku ndani ya jamii. Pia, imedhihirisha uwepo wa sauti nyingi zilizo huru. Barua hizo saba ni sauti kutoka kwa waandishi wa barua hizo nje ya sauti ya mwandishi wa riwaya hiyo. Hakuna matini inayoweza kujitegemea bila uwepo wa matini nyingine (Bakhtin, 1981).

Pia, data za utafiti kutoka riwaya ya kiwasifu ya *Mikidadi wa Mafia, Maisha ya Mwanaharakati na Familia yake nchini Tanzania* (2014) imedhihirisha matumizi ya barua za kiofisi na barua za kirafiki. Katika riwaya hii, barua za Mikidadi alizomwandikia Caplan wakati alipokuwa nchini Uingereza zimechopekwa katika hadithi kuu. Miongoni mwa barua hizo ni kama ifuatavyo:

> *20/5/67. Mikidadi Juma, H.S. P. S (Haile Selassie* Primary School
> Kwa dada yangu mpendwa A. P. Baley,
> Salamu nyingi sana ama baada ya salamu kwanza natumaini kujua hali yako na uzima wako na upendapo kujua hali yangu mimi mzima. Madhumuni ya barua hii ni kwanza kukujulisha kuwa, barua zako zote nimezipata na picha nimezipata. Nina huzuni kukujulisha kwamba mzee Omary bin Masharubu amefariki. Na nimefurahi kusikia kwamba umenunua nyumba. Na mimi ningependa kukuuliza je utakuja tena Mafia au Unguja? Je, unaendelea kusoma masomo gani sasa? Mimi ningalipo hapa Unguja ninaendelea na masomo yangu lakini natumaini nitaenda Mafia hivi karibuni.....*Mr* Abdallah anakuomba umposee mtoto mmoja wa kizungu, pia anasema anataka kuja Ulaya lakini anasema atakupata vipi? Nategemea utakuja kunichukua na mimi nikuone

> Ulaya. Majibu haraka. Wanakusalimu wazee wa Mafia na wote kwa ujumla. *Please I need your help. To see you day one. Yours* (Caplan, 2014:14).

Data hii ni barua halisi iliyoandikwa na Mikidadi mnamo tarehe 20/5/67 kwenda kwa Caplan ili kumjulisha kuwa amezipokea barua zote ambazo alikuwa amemwandikia. Hii ni barua ya kirafiki. Barua hii imeanza na salamu, kisha kiini cha barua, na hitimisho. Mwisho wa barua hakuna jina bali mwandishi ametumia kiwakilishi kimilikishi "*yours*". Mwandishi ametumia barua hii kuwasilisha hali halisi ya ustawi pamoja na changamoto za Mikidadi, familia yake na wanajamii wa Kisiwa cha Mafia. Mawazo ya Bakhtin (1981) yamedhihirika katika riwaya hii, kwani mtaalamu huyu anaeleza kuwa kazi ya fasihi inahusisha njia mbalimbali za mawasiliano ya kila siku ndani ya jamii yaliyojumuishwa katika hadithi kuu na kuunda riwaya nzima. Aidha, hakuna matini inayoweza kujitegemea bila kuwepo kwa matini nyingine.

Vilevile, data za utafiti kutoka katika riwaya ya *Maji Hayafuati Mkondo* (2018), zimedhihirisha matumizi ya barua katika hadithi kuu, mathalani, barua kutoka kwa Sami kwenda kwa Sinta kama ifuatavyo:

> Dear Sinta,
> Nimejitahidi tuwe na maongezi japo ya nusu saa, lakini imeshindikana. Naona umeshikilia msimamo wako. Sinta mimi sina nia ya kukuharibia. *Yes!* Nakubali nimeharibia wengi lakini amini kuwa sitakuharibia maisha yako. Sinta nakupenda. *I am very serious about this.* Tafadhali nipe nafasi. Mimi nataka tuweke malengo ya muda mrefu. Ninakuhakikishia sitakuudhi wala kukukwamisha. Tafadhali fikiria ombi langu. Najua ni mama anayewajibika na hataki mwanae apotee. Tafadhali Sinta, nipe nafasi.
> *I love you,*
> Sami
> (Mahonge, 2018: 34)

Dondoo la barua hii linadhihirisha matumizi ya barua ya kubuni ambayo ni ya kirafiki. Barua imeanza na salamu: "*Dear* Sinta" halafu kiini na mwisho imehitimishwa kwa Kiingereza "*I love you*" na kuandikwa jina la mwandishi. Barua hii ni maombi ya urafiki wa kimapenzi. Pia, barua hii imechanganya Kiingereza na Kiswahili: "*Yes! I am very serious about this, I love you*". Pia, katika barua hii tunabaini msisitizo katika aya ya kwanza, "Nimejitahidi tuwe na mazungumzo japo nusu saa, lakini imeshindikana." Aidha, msisitizo huo umeendelezwa katika aya ya pili, "Tafadhali nipe nafasi. Tafadhali fikiria ombi langu. Tafadhali Sinta nipe nafasi". Barua hii pamoja na barua nyingine mbili zimetumika katika hadithi kuu ya riwaya hii. Hali hii inathibitisha kuwa hakuna matini inayoweza kujitegemea bila

kuwepo kwa matini nyingine (Bakhtin, 1981). Pia, tumeshuhudia matumizi ya mawasiliano ya kila siku katika jamii ambayo yametumika kama sehemu ya mtindo katika riwaya hiyo.

### 5.2 Mtindo wa Shajara

Zaidi ya mtindo wa barua hapo juu, data za utafiti huu zimebaini kutumiwa kwa mtindo wa shajara katika riwaya teule mbili kati ya nne zilizoteuliwa. Riwaya hizo ni *Mikidadi wa Mafi: Maisha ya Mwanharakati na Familia yake Nchini Tanzania* (2014), na *Kolonia Santita* (2017) kama Jedwali Na. 2 linavyoonesha:

**Jedwali Na. 2: Data kuhusu Utokeaji wa Shajara katika Riwaya Teule**

| **Riwaya Teule** | **Shajara** | **Kategoria** | **Taarifa katika Shajara** |
|---|---|---|---|
| *Mikidadi wa Mafia: Maisha ya Mwanaharakati na Familia yake Nchini Tanzania* (2014) | 8 | Halisi | Rasmi na zisizo rasmi |
| *Kolonia Santita* (2017) | Madondoo 8 ya shajara | Shajara ya kibunifu | Rasmi na zisizo rasmi |

**Chanzo:** *Mikidadi wa Mafia: Maisha ya Mwanaharakati na Familia yake Nchini Tanzania* (2014) na *Kolonia Santita* (2017)

Utafiti huu umebaini matumizi ya shajara nane katika riwaya ya *Mikidadi wa Mafia: Maisha ya Mwanaharakati na Familia yake Nchini Tanzania* (2014). Mwandishi, Pat Caplan, akisimulia maisha ya mhusika Mikidadi ametumia nukuu za shajara halisi ambazo Mikidadi alitumia katika maisha yake kama ifuatavyo: "Kwa vile baadhi ya matukio hayo hivi sasa hayapo tena, napenda ninukuu matukio mawili ya Mwaka Kogwa na yale ya jando ambayo Mikidadi aliandika katika shajara yake". Mojawapo ya shajara iliyochopekwa katika riwaya hii ni kama ifuatavyo:

**Kumbukumbu ya Mikidadi ya Tukio la Mwaka Kogwa la 1966**

31/7/66. IDI YA MWAKA: Vikao vya mwaka: Changwa watu 35, Rasini watu 50

CHAKULA: Mikate ya Pwani

Nyimbo walizoimba: Mwaka (Bt Ali), Ile (Bt Khalidi), (Bt Hija), na Liwale (Bt. Ali)

Vitu wanavyochukua pwani: wanawake- vijiti vya mvinje au matawi: wanaume – fimbo za kupigania, huku wakisema "mwaka hauna sharia"

SHEREHE: Mahali pa Bw. Kingunu Sonondo (Pindi). Wachezaji (watoto wadogo na watu wazima wanawake)

1/8/66. SHEREHE: Siku ya 2: Mahali pa Bw Kigunu. Njoma (1) Mkwaju (2) Sondo/ Pili

> Sonondo watoto wadogo na watu wakubwa na vile vile mkwaju. Kiasi cha watu 410 wazee na watoto. Waliosikiwa (1) Mzee Kingume.
> 2/8/66: Kumaliza Idi. Ngoma Sondo/pindi. Wachezaji watoto wadogo 90, kiasi cha watoto (wa kiume) 100.
> (Caplan, 2014:11).

Kupitia madondoo hayo, tumebaini matumizi ya shajara halisi yenye taarifa binafsi kuhusu matukio katika jamii ya Wanamafia. Aidha, shajara imeanza na kichwa cha habari, tarehe za matukio, wahusika na matukio yaliyofanyika. Shajara hii ilikuwa ya Mikidadi yenye kumbukumbu za matukio halisi yaliyotokea wakati wa uhai wake. Matumizi ya madondoo 8 ya shajara katika hadithi kuu, yanadhihirisha matumizi ya mawasiliano ya kila siku ndani ya jamii kama ilivyo katika mtindo wa barua. Mitindo yote huingiliana na kuunda riwaya nzima (Bakhtin, 1981).

Pia, utafiti huu umebaini matumizi ya mtindo wa kiepisto unaohusisha shajara katika riwaya ya kipelelezi ya *Kolonia Santita* (2018). Riwaya hii nzima imeandikwa kutoka mwanzo mpaka mwisho kwa mtindo wa shajara. Dondoo la kwanza la shajara lilihusu kikao cha dharura kama ifuatavyo:

> KIKAO CHA DHARURA
> Jumatano, 28/10/1992. 10:17 alasiri.
> Kiongozi wa Kanda ya Afrika ya Kusini ya Tume ya Dunia ya Kudhibiti Dawa za Kulevya Kamishna Profesa Justin Mafuru wa Tanzania, 59, alikuwa na shughuli nyingi alipoitwa na mwanafunzi wake kupokea simu ya Mkurugenzi wa Sekretariet ya Kanda ya Afrika ya Kusini ya Tume ya Dunia Mohammed Nafi. Nafi katika simu, alimsihi profesa wakutane haraka katika ofisi ya Tume kupokea ujumbe uliofika jioni hiyo kutoka *Olso*, Norwei, Skandinavia.
> Kamishna, Profesa wa Fizikia na kinara wa mionzi ya *gamma rays pioneer* aliyekuwa akiiwakilisha Tanzania katika shirika la utafiti wa nyuklia la Bara la Ulaya (CERN) nchini Uswisi katika jitihada za kujibu maswali mazito kabisa ya mlipuko wa *Big Bang*. Alitoka katika Maabara ya Fizikia ya Chuo Kikuu cha Dar es Salam na kukaa nyuma ya usukani wa gari lake jipya…..Saa 10:50 jioni, nusu saa tangu atoke katika ofisi yake ya Chuo Kikuu, Profesa alikuwa akiingiza gari lake katika maegesho maalumu ya ofisi ya Tume Barabara ya Samora, Dar es Salaam, Tanzania... (Malegesi, 2017: 1).

Kupitia dondoo hilo, data zinadhihirisha matumizi ya dondoo la shajara lenye taarifa za kiofisi kuitwa kazini Profesa Justin Mafuru. Dondoo la shajara lina kichwa cha habari, "KIKAO CHA DHARURA". Baada ya kichwa cha habari, imeandikwa siku, "Jumatano", tarehe "28/10/1992" saa "10:17 Alasiri" na mahali

mhusika alipokuwapo, yaani "Maabara ya Fizikia ya Chuo Kikuu cha Dar es Salam na ya ofisi ya Tume iliyoko Barabara ya Samora, Dar es Salaam, Tanzania". Matumizi ya madondoo 8 katika hadithi kuu yanadhihirisha matumizi ya mawasiliano ya kila siku ndani ya jamii kujumuishwa katika hadithi kuu na kuunda riwaya nzima. Kama ilivyodokezwa hapo juu, hakuna matini inayoweza kujitegemea bila kuwepo matini nyingine (Baktin, 1981).

### 5.5 Mtindo wa Baruapepe

Riwaya *Mikidadi wa Mafia: Maisha ya Mwanaharakati na Familia yake Nchini Tanzania* (2014), imedhihirisha matumizi ya baruapepe kama jedwali linavyoonesha:

**Jedwali Na. 3: Data kuhusu Utokeaji wa Baruapepe katika Riwaya Teule**

| **Riwaya Teule** | **Idadi ya barua** | **Kategoria** | **Aina za barua** |
|---|---|---|---|
| *Mikidadi wa Mafia: Maisha ya Mwanaharakati na Familia yake Nchini Tanzania* (2014) | 5 | Halisi | ya kirafiki |

**Chanzo:** *Mikidadi wa Mafia: Maisha ya Mwanaharakati na Familia yake Nchini Tanzania* (2014)

Katika dondoo hilo, Pat Caplan, mwandishi wa riwaya hii, ameelezea maisha ya mhusika Mikidadi, kwa kutumia nukuu za baruapepe halisi ambazo alizipokea kutoka kwa watu mbalimbali baada ya kifo cha Mikidadi kama ifuatavyo:

> Baadaye nilipokea baruapepe ambazo wakati huo ni watu wachache tu ndio walikuwa wanatumia njia hiyo katika mwaka 2002. Mojawapo ilitokea kwa mwanachama wa CHAMAMA ambaye nilimtumia baruapepe kuuliza habari za mazishi.
>
> 5/12/02. Yaliyozungumzwa baada ya msiba, kwanza ni kuwajulisha watu muhimu. Pia Kamati Kuu ya CHAMAMA imekubaliana itafute fedha ili kusaidia familia pamoja na kuangalia kama kuna madeni ili yalipwe. Kwa kipindi hiki familia yake imekwenda Mafia kwa msiba kwa muda wa siku arobaini.
>
> 19/12/02. Kwa kweli kama ulivyosema katika barua yako ya tarehe 25/11/02 ya kuwa marahemu alikuwa mtu mwema sana kwa wenzake, na hili pengo alilotuachia sasa ni wajibu wetu sisi kulijaza kwa sababu kitu kizuri tusikubali kukiacha kikapotea. Maana yangu nakusudia kusema mambo aliyokuwa akiyafanya marehemu tuyaendeleze. (Caplan, 2014:127)

Madondoo hayo yanadhihirisha matumizi ya baruapepe za kirafiki. Mwandishi hakuweka anwani ya baruapepe hizo, ila ametaja tarehe ambazo baruapepe ziliandikwa. Baruapepe hizi hazina majina ya waandikiwa wala walioandika, isipokuwa wametajwa na mwandishi katika usimulizi wake. Kwa mtazamo wetu, barupepe hizo hazina tofauti na barua za kawaida; zimetumika kutoa pole kwa Chaplan kwa kifo cha Mikidadi. Baruapepe hizo, zimezungumzia mambo makuu mawili: mosi, ni taarifa ya msiba wa Mikidadi, na pili, ni salamu za rambirambi kwa familia ya Mikidadi. Aidha, baruapepe hizo zimetumiwa kueleza maisha ya Mikidadi, hususani tabia yake ya wema. Baruapepe zote zimeandikwa na watu tofauti kwenda kwa Caplan. Baruapepe hizo ziliandikwa mwaka 2002. Hivyo, kwa mtazamo wetu, yawezekana huo ndio wakati ambapo mitindo ya matumizi ya mawasiliano ya kiektroniki yalipoanza kutumika katika kazi za fasihi. Matumizi ya barua katika riwaya hii yanadhihirisha kuwapo kwa njia za mawasiliano yenye sanaa ya kiwango cha juu kutoka kwa mwandishi zenye uzungumzi nafsi wa wahusika. Baruapepe hizo zimejumuishwa katika hadithi kuu na kuunda riwaya nzima (Bakhtin, 1981).

## 6.0 Lugha Iliyotumika katika Mitindo ya Kiepisto

Katika utafiti huu, tumebaini matumizi kadhaa ya lugha ya kisanaa ambayo yanaifanya mitindo hii kuwa na mchango katika kujenga ufasihi wa riwaya teule. Vipengele vya lugha tulivyovibaini katika mitindo hiyo ni tasfida, majazi, tashibiha, taashira au mubalagha, nahau, misemo na methali. Katika makala haya, mfano mmoja utatolewa kwa kila aina ya kipengele cha matumizi ya lugha kilichojitokeza katika riwaya teule ili kuwakilisha vipengele vingine vinavyofanana na hivyo. Hebu tuangalie mifano hiyo ya matumizi ya lugha katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na. 4: Tamathali za Usemi, Methali Nahau na Misemo**

| **Riwaya Teule** | **Tamathali za Usemi** | **Aina** |
|---|---|---|
| *Dunia Uwanja wa Fujo* (2007) | *Moyo wangu* ulikuwa na *njaa yako*, vile kwamba sikuweza kuvumilia (uk. 68).<br>Wakati ninapoandika barua hii nimechukua *mali yako tumboni* mwangu (uk. 68). | tasfida |
| | Labda *maji ya bahari* yamekufanya uwe mweupe vile (uk. 68).<br>Umenisimamisha juu ya *jukwaa nikiwa uchi* ili ulimwengu upate kunicheka (uk. 110). | majazi |
| | Umenifukuza *kama mbwa* (uk. 68). | tashibiha |
| | Nachimba udongo (uk. 123).<br>Ninaishi ndani ya mapipa (uk. 123). | misemo |
| *Mikidadi wa Mafia: Maisha ya Mwanaharakati na* | Kwa ajili ya kuvaa kwenye party *mitoko miwili* (uk. 17).<br>Alimweka *kiti moto* na kuelezwa kuna | misemo |

| **Riwaya Teule** | **Tamathali za Usemi** | **Aina** |
|---|---|---|
| *Famili yake Nchini Tanzania* (2014) | malalamiko (uk. 116). | |
| | Mkuu wa Wilaya alimjibu nina *mkono mrefu* (uk. 116). | nahau |
| *Kolonia Santita (2017)* | Nukta ileile akitoa mapigo makali *mbwa mwizi* (uk. 30). | sitiari |
| | *Matako yakitingishika* kama *yanaumwa kifafa* (uk. 34).<br>*Aliruka kama nyani* na *kutua kama ndege* juu ya mwili wake (uk. 152). | tashibiha |
| | Wahenga walisema ulimi *hauna mfupa* (uk. 39)<br>Alikiona cha mtema kuni (uk. 140) | nahau |
| | *Machale yalianza kumcheza* Radia (uk. 45).<br>Kila mtu alikuwa na *hamsini zake* (uk. 50) | misemo |
| | Siku za mwizi arobaini (kur. 223 na 352).<br>Majuto ni mjukuu (uk. 241).<br>Asiyesikia la mkuu huvunjika mguu (uk. 263). | methali |
| *Maji Hayafuati Mkondo (2018)* | Tangu uanze *kuwabadilisha kama mashati* mpaka leo umefaidika kwa kiasi gani (uk. 173). | tashibiha |
| | *Kila hatua nitakayopiga* ni kwa ajili yako na familia yetu wote (uk. 173). | msemo |

**Chanzo:** *Dunia Uwanja wa Fujo, Mikidadi wa Mafia: Maisha ya Mwanaharakati na Famili yake Nchini Tanzania, Kolonia Santita na Maji Hayafuati Mkondo*

### 6.1 Matumizi ya Tasfida

Tasfida ni maelezo yanayolenga kupunguza makali ya maneno. Lengo la matumizi ya tasfida ni kuonesha heshima (Madumulla, 2022). Matumizi ya tasfida katika kazi za fasihi hudhihirisha sanaa ya matumizi ya lugha. Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), matumizi ya tasfida yamejitokeza katika mtindo wa episto barua katika barua ya Vera aliyomwandikia Dennis kama ifuatavyo:

> ...Lakini Dennis! Siku niliyokuona huko mjini Dar es Salaam ulikuwa umekwisha badilika. Ulikuwa mzuri sana machoni mwangu. *Moyo wangu ulikuwa na njaa yako* vile kwamba sikuweza kuvumilia. Nilitoa *cho chote nilikuwanacho*. Labda *maji ya bahari ndiyo yamekufanya uwe mweupe vile*! Dennis mambo yalitendeka Rex Hotel. Wakati ninapokuandikia barua hii *nimechukua mali yako tumboni mwangu*. Ukinitupa sasa, basi, maisha yangu yameharibika

> Sina mengi, pokea picha yangu. V*”* (Kezilahabi, 2007: 68)

Kulingana na dondoo hilo, tasfida “*Moyo wangu ulikuwa na njaa yako”* imetumika kuonesha heshima katika kuelezea hamu aliyokuwanayo Dennis ya kufanya mapenzi na Vera. Katika hali ya kawaida moyo hauwezi kusikia njaa, bali moyo unadhihirisha hisia za mtu. Njaa huwa ni hisia ya mtu kwa ajili ya uhitaji wa kupata chakula na si jambo jingine. Aidha, katika barua hiyo kuna tasfida, “*nimechukua mali yako tumboni mwangu*”. Mali ni bidhaa ambayo huuzwa madukani wakati tumbo ni sehemu ya mwili wa binadamu. Mali kuwamo katika tumbo la binadamu inamaanisha kitu cha thamani. Katika muktadha huu, tunabaini ukiushi wa maana katika matumizi ya tasfida. Vera anamaanisha kuwa ni mjamzito. Ujauzito mwisho wake ni kuzaa mtoto. Mtoto ni kiumbe wa thamani kubwa, hawezi kulinganishwa na bidhaa ambayo inapatikana mahali popote.

### 6.2 Matumizi ya Majazi

Majazi ni tamathali inayohusu kitu au mnyama kusimama badala ya kitu kingine (Madumulla, 2022). Majazi hutumika katika kazi za fasihi kudhihirisha sanaa iliyomo katika kazi hiyo. Katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975) matumizi ya majazi yamedhihirisha sanaa katika mtindo wa episto barua katika barua Vera aliyomwandikia Dennis kama ifuatavyo:

> Denis,
> Asante sana. Umenifukuza kama mbwa *Umenirudisha nyumbani na lubega ingawa uliniona nikiwa na nguo nyingi*. Umeniondolea heshima yangu. Dennis *umenisimamisha juu ya jukwaa nikiwa uchi ili ulimwengu upate kunicheka*. Asante sana... Dennis sina mengi ya kusema maana shauri umekwisha kata. Kuomba msamaha naona aibu… Kwa huruma yako nakuomba! Mimi sitakusahau: Hata kama nikifa nitamwomba Mungu akusamehe.
> *Ninakutakia maisha marefu na hao warembo.*
> Wako daima
> (Bibi) Dennis
> (Kezilahabi, 2007: 110)

Dondoo hapo juu linadhihirisha matumizi ya majazi katika barua ya Vera kwenda kwa Dennis: “*Umenirudisha nyumbani na lubega ingawa uliniona nikiwa na nguo nyingi*”, *“…umenisimamisha juu ya jukwaa nikiwa uchi ili ulimwengu upate kunicheka”*, pamoja na “*Ninakutakia maisha marefu na hao warembo*.” Neno “*lubega”* ni aina ya uvaaji ambao shuka au kitenge huvaliwa kwa kupitishwa chini ya kwapa la mkono mmoja na kufungwa fundo juu ya bega la mkono mwingine (BAKITA, 2015). Neno juu ya “*jukwaa*” linamaanisha hadharani, na neno “*uchi*” limesimama badala ya hali ya stara ya aina yoyote. Aidha, neno warembo maana yake ni wanawake wazuri. Majazi yametumika kupunguza makali ya maneno halisi

yanayowasilisha hali hizo. Kwa kuzingatia Nadharia ya Mtindo, tunaona jinsi matumizi ya majazi yalivyoathiri maana kama inavyofasiriwa katika hali ya kawaida. Neno "*jukwaa*" katika hali ya kawaida ni sehemu ya kuoneshea matukio mbalimbali, lakini katika barua hii, maana yake imebadilika na kuwa hadhira.

**6.3 Matumizi ya Tashibiha**

Tashibiha ni maelezo ambayo hukipa kitu au mnyama sifa za binadamu. Vitu au wanyama hao, hutenda kama binadamu (Madumulla, 2022). Matumizi ya tashibiha ni mbinu ya kudhihirisha sanaa katika kazi ya kifasihi. Katika riwaya ya *Kolonia Santita* (2017) matumizi ya tashibiha yamedhihirisha sanaa katika mtindo wa episto shajara katika dondoo la nne la shajara zilizosimulia matukio ya oparesheni ya Kolonia Santita kama ifuatavyo:

> Baada ya kumpongeza mkurugenzi wa usalama wa kazi ile kubwa ya muhimu, Murphy aliwagawa watu wake. Radia alielekea mashariki wakati Monges na Yehuda wakienda kusini na magharibi kwa mfuatano huo: na Murphy akikimbilia kaskazini katika geti kubwa la chuma. *Kila mmoja katika upande wake alinyata kama chui,* katika jitihada za kumnasa mlinzi wake... Machale yalimcheza halafu akakamata bunduki sawasawa na kuanza kutembea kwa hatua za haraka kurudi alikokuwa mwanzo. Pengine alisikia vibaya, huenda hakusikia mluzi. Lakini, kabla hajavuta hatua mbili au tatu hivi, mlinzi alikiona cha mtema kuni! Radia *aliruka kama nyani na kutua kama ndege* juu ya mwili wake, wote wakaenda chini ka kishindo!
> (Maregesi, 2017: 151 -152).

Katika dondoo hapo juu, matumizi ya tashibiha yamebainishwa katika italiki. Tashibiha hizi mbili zinatoa taswira ya namna Vijana wa Tume (Murphy, Monges, Yehuda na Radia) walivyotembea wakati wanaelekea kuwatafuta maadui zao ambao walikuwa katika jengo la Kolonia Santita kambi ya *Copenhargen* Denmaki. Mwandishi amefananisha mnyama "*chui"* anavyotembea anaponyatia windo lake na Vijana wa Tume walivyowanyatia maadui zao. Pia, amefananisha jinsi "*nyani*" anavyoruka na "*ndege*" anavyotua kutoka juu na jinsi Radia alivyoruka na kutua juu ya mwili wa mlinzi ambaye alikuwa akimvizia kama ndege. Taswira ya namna chui anavyotembea, nyani anavyoruka na ndege anavyotua imejenga picha ya hali halisi kwa msomaji kuhusu jinsi Radia alivyokuwa anapambana na maadui zake. Matumizi ya tashibiha katika dondoo la shajara yanadhihirisha matendo ya binadamu kufananishwa na wanyama. Katika hali ya kawaida si rahisi binadamu kutenda kama myama, kunyata kama chui, kuruka kama nyani, na kutua kama ndege.

### 6.4 Matumizi ya Sitiari

Sitiari ni maelezo yanayolinganisha na kuhusisha vitu viwili tofauti kitabia na kimaumbile. Maana na hisia ya kitu kimoja huhamishwa kwenye kitu kingine (Madumulla, 2022.) Matumizi ya sitiari yamejitokeza katika riwaya ya *Kolonia Santita* (2017), na kudhihirisha sanaa katika mtindo wa episto shajara. Mwandishi ametumia sitiari katika dondoo la kwanza la shajara lililosimulia matukio ya Vijana wa Tume kama ifuatavyo:

> Siku moja, John alihudhuria sherehe ya ndugu yake katika ukumbi fulani huko Kariakoo, Dar es Salaam... Lakini, baada ya saa moja hivi tangu shughuli zianze majambazi watano walivamia ukumbi na kusababisha fujo ya hali ya juu. Bila kupoteza muda, John Ambilikile alivuta pumzi. Aliposhusha watu walishangaa aliporudisha punje za matumaini yao kwa umahiri na ufundi wa hali ya juu. Alikwepa visu, mapanga na miti, huku nukta ileile akitoa mapigo makali ya *mbwa mwizi* na dakika chache akawa amwashida wote bila yeye kuwa na jeraha hata moja katika mwili wake (Malegesi, 2017: 30).

Katika dondoo hapo juu, mwandishi ametumia sitiari "*mapigo makali ya mbwa mwizi*." Mbwa ni mnyama ambaye hutumika kwa shughuli za ulinzi na uwindaji katika jamii nyingi. Lakini wakati mwingine huwa si rafiki wa binadamu. Mbwa anapokuwa mwizi watu humshambulia bila huruma. Hivyo, sitiari hii inatoa taswira ya shambulio kali kama vile ambavyo mbwa mwizi huwa anashambuliwa na watu. Hivyo ndivyo Ambilikile alivyowashambulia majambazi waliofanya vurungu katika sherehe ya rafiki yake iliyofanyika katika ukumbi mmoja Kariakoo, jijini Dar es Salaam. Matumizi ya sitiari yanadhihirisha matumizi ya tamathali za semi yanavyodhirisha sanaa iliyomo katika lugha iliyotumika katika dondoo la shajara.

### 6.5 Matumizi ya Nahau

Nahau ni maneno ya kawaida yenye maana ya kificho ambayo hutumika kutoa ujumbe kwa njia ya kificho ili kuiasa jamii (Mulokozi, 2017). Matumizi ya nahau katika kazi za fasihi yanalenga kuonesha sanaa katika kazi hiyo. Katika riwaya ya *Mikidadi wa Mafia: Maisha ya Mwanaharakati na Familia yake Nchini Tanzania* (2014), matumizi ya nahau yamedhihirika katika mtindo wa episto shajara. Nahau zimejitokeza katika shajara ambayo Mikidadi alinukuu changamoto alizokutana nazo wakati akiwa kiongozi wa asasi ya kiraia ya Changia Maendeleo ya Mafia (CHAMAMA) kama ifuatavyo:

> Alielezwa kuwa kuna malalamiko kuhusu yeye Mikidadi alimuuliza: "ushahidi gani unao kuhusu hayo? Huwezi tu kusema mambo kama hayo!"
> Mkuu wa Wilaya alimjibu "*Nina Mkono Mrefu*!" Walitumia muda mwingi karibu masaa matatu na mwisho Mkuu wa Wilaya

> alimwomba msamaha kwa kusema: “Sina ninalomudu kulifanikisha hapa (Mafia), kila kitu kinakwama (Caplan, 2014: 115-116).

Dondoo hapo juu, linadhihirisha matumizi ya nahau “*nina mkono mrefu*”. Anayetumia nahau hiyo ni Mkuu wa Wilaya wakati akizungumza na Mikidadi. Kulingana na wadhifa alionao katika wilaya yake, yeye ndiye mwakilishi wa serikali katika wilaya hiyo. Hivyo, kauli yake inamaanisha serikali ipo kila mahali na ina uwezo wa kumfikia mtu yeyote mahali popote. Katika dondoo la shajara, tunabaini matumizi ya nahau “*nina mkono mrefu*” ambayo maana yake imefichika. Haya ni matumizi ya ukiushi wa maneno kwa njia ambazo si za kawaida (Leech, 1969; Wamitila, 2008).

**6.6 Matumizi ya Misemo**

Misemo ni semi zinazoibuka kwa muda fulani kwa madhumuni maalumu na kuonekana katika jamii na kisha kutoweka au kubadilika katika kumbukumbu za watu kwa muda mrefu (Mulokozi, 2017). Dhima ya misemo katika kazi za fasihi ni kuonesha sanaa katika kazi hiyo. Misemo imejitokeza katika riwaya ya *Kolonia Santita* (2017) katika dondoo la nne la shajara kama ifuatavyo:

> *Machale yalimcheza* halafu akakamata bunduki sawasawa na kuanza kutembea kwa hatua za haraka kurudi alikokuwa mwanzo. Pengine alisikia vibaya huenda hakusikia mluzi. Lakini, kabla hajavuta hata hatua mbili au tatu hivi, mlinzi *alikiona cha mtema kuni*! (Maregesi, 2017: 152)

Dondoo hapo juu linaonesha matumizi ya misemo “machale yalimcheza” na “alikiona cha mtema kuni”. Misemo hii miwili imetumika kusimulia jinsi Radia alivyopambana na mlinzi ambaye alikuwa analinda getini. Mlinzi machale yalimcheza alipogundua kuna dalili ya kuwa wamevamiwa. ‘Machale kucheza’ ni hali ya wasiwasi inayompata mtu anapohisi kuna jambo la hatari linamjia. Baada ya muda mfupi mlinzi ‘alikiona cha mtema kuni’, msemo huu unamaanisha alipigwa vibaya sana na Radia. Matumizi ya misemo katika dondoo la shajara yanadhihirisha jinsi matumizi ya lugha yanavyoathiri maana. Ukiushi wa aina hii si wa kawaida kimaana kama inavyofasiriwa katika hali ya kawaida (Leech, 1969; Wamitila, 2008). Kutema kuni ni kitendo cha kutumia shoka na kukata gogo la mti ili kupata kuni kwa ajili ya kupikia. Kukata kuni ni kazi inayohitaji nguvu na inayochosha. Hivyo, imefananishwa na hali ngumu iliyomkabili mlinzi.

**6.7 Matumizi ya Methali**

Methali ni usemi mfupi wa mapokeo unaodokeza kwa muhtasari fikra au mafunzo mazito yaliyotokana na tajiriba ya jamii inayohusika (Mulokozi, 2017). Katika riwaya ya *Kolonia Santita* (2017), dondoo la saba la shajara linalosimulia

mapambano baina ya Vijana wa Tume na genge la Kolonia Santita la Meksiko limedhihirisha matumizi ya methali kama ifuatavyo:

> Murphy alishindwa kujua nini kilikuwa kinaendelea. Walinzi walionekana kudhuriana wao kwa wao! Kwa nini? Kwa nini huyo mlinzi amuue mwenzake? Nani ameua wale wawili na nje? Labda mwenzake aliona upuuzi na hivyo kumuua! Hata hivyo, *pilipili usizozila zakuwashia nini*? Murphy aliamua kuachana na ugomvi wao na kutembea haraka ili akutane na yule mlinzi mbabe (Malegesi, 2017: 286).

Dondoo hapo juu linadhihirisha matumizi ya methali "*pilipili usizozila zinakuwashia nini*." Mwandishi ametumia methali hii kwenye shajara ya saba katika riwaya husika kuonesha mawazo aliyokuwa nayo Murphy ambaye alikuwa akijiuliza maswali kadhaa kuhusu kilichokuwa kinaendelea baina ya walinzi. Hata hivyo, hakutaka kujishughulisha na ugomvi huo kwa sababu pilipili asizozila mtu hazipaswi kumuwasha. Matumizi ya methali katika dondoo la shajara yanadhihirisha matumizi ya lugha ya kificho ambayo maana yake haiko wazi. "*Pilipili usizokula zinakuwashia nini*" katika hali ya kawaida ungeweza kusema kwa nini uhangaike na jambo lisilokuhusu. Huu ni ukiushi unaohusu matumizi ya maneno kwa njia ambazo si za kawaida kimaana kama inavyofasiriwa katika hali ya kawaida (Leech, 1969; Wamitila, 2008).

**7.0 Hitimisho**

Makala haya yamechunguza mitindo ya kiepisto katika fasihi ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti wetu yamedhihirisha Kezilahabi (2007) ametumia barua chache ndani ya hadithi kuu. Caplan (2014) ametumia arafa, barua, baruapepe na shajara katika hadithi kuu. Malegesi (2017) ametumia madondoo ya shajara kujenga hadithi kuu na Mahonge (2018) ametumia barua chache ndani ya hadithi kuu. Kutokana na matokeo hayo, tunashuhudia kila mwandishi ametumia mtindo au mitindo ya kiepisto kwa namna yake. Hivyo, riwaya inaweza ikahusisha mtindo mmoja au zaidi ya mtindo mmoja katika riwaya moja. Makala haya yamebaini mitindo ya kiepisto iliyotokana na mawasiliano ya kawaida ya kila siku ya barua na shajara. Vilevile, mtindo uliotokana na mawasiliano ya kielektroniki wa baruapepe umejitokeza katika riwaya teule moja kati ya nne zilizoteuliwa. Mitindo mingine ya mawasiliano ya kielektroniki kama arafa na blogu haikudhihirika bayana ingawa imetajwa kutumika. Aidha, utafiti huu umeelezea vipengele vya matumizi ya lugha vilivyojitokeza katika mitindo hiyo. Vipengele hivyo ni tasfida, tashibiha, sitiari, dhihaka, majazi, methali, misemo na nahau. Kwa mantiki hiyo, ni wazi kuwa mitindo ya kiepisto ina sifa na vigezo vya kuweza kujumuishwa miongoni mwa mitindo ya uandishi wa kazi za fasihi.

**Marejeleo**

Aşci, Y. (2020) "Letter Tradition and Epistolary Novel in American Literature". *The Journal of International Social Researc*h, Juz. 13 (74): 5-12. Ilipatikana katika https://www.sosyalarastirmalar.com/articles/letter-tradition-and-epistolary-novel-in-american-literature.pdf. Ilisomwa tarehe 10 Januari 2022.

Bakhtin, M.M. (1981) *The Dialogic Imagination: Four Essays*. Austine: University of Texas Press.

Caplan, P. (2014) *Mikidadi wa Mafia: Maisha ya Mwanaharakati na Familia yake Nchini Tanzania* (Imefasiriwa na A. Kipacha). Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Couldry, N. na Mc Carthy, A. (2004) *Mediaspace, Place, Scale and Culture in a Media Age*. New York: Routledge.

Crystal, D. na Davy, D. (1981) *Investigating English Style*. London: Longman.

Dagel M. J. (2012) "*The Influence of Digital Communication on Young Adults Contemporary Fiction"* Ilipatikana katika https://scholarworks.uni.edu/grp/12 Ilisomwa tarehe 12 Juni 2023.

Holoquist, M. (1990) *Dialogism: Bakhtin and His World*. London: Routledge.

Jilala, H. (2016) *Misingi ya Fasihi Linganishi, Nadharia, Mbinu na Matumizi*. Dar es Salaam: Daudi Publishing Company.

Kezilahabi, E. (2007) *Dunia Uwanja wa Fujo*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Leech, G. N. (1969). *A linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman Group Ltd.

Leech, G. N. & Short, M. (2007) *Style in Fiction: A lingustic Introduction to English Fictional Prose*. Lancaster: Longman Group LTD.

Madumulla, J. (2022) *Riwaya ya Kiswahili, Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. (Toleo la 2) Dar es Salaam: Afroplus Industries LTD.

Mahonge, F. R. (2018) *Maji Hayafuati Mkondo*. Dar es Salaam: Africa Proper Education Network.

Malegesi, E. (2017) *Kolonia Santita*. Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Morson, C. (1986) *Bakhtin Essays and Dialogues of His Work*. Chicago: The University of Chicago Press.

Mulokozi, M.M. (2017) *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu*. Dar es Salaam: KAUTTU Publishers.

Mutembei, A.K. (2016) "Epistolary role in East African literary works on HIV/AIDS". *A Journal of the University of Namibia Language Centre*, Juz. 1 (1): 100 – 115.

Mwansoko, H. (1991) *Mitindo ya Kiswahili Fasaha*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Njogu, K. (2004) *Reading Poetry As Dialogue*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Ondus S.M. (2014) *Writing About Writing: African Women Epistolary Narratives*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Connecticut, Connecticut.

Senkoro, F.E.M.K. (2011) *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.

Simpson, P. (2004) *Stylistics A Resource Book for Students*. London: Routledge.

Vinogradu, A. na Skuortson, L.V. (2014) "Information Needs and Information Culture, Theory and Practice of Social – Scientific Information" 4, 4-5, Juz. 11(5)1305-1319. Belarus: University of Belarus.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Walibora, K. W. (2010) "Uhalisia na Uhalisia Mazingaombwe: Mshabaha kati ya Dunia Yao na The Tin Drum". *Swahili Forum* 17: 143- 157.

Wamitila, K. (2008) *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Limited.